**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**WILAYA YA SIHA - SHULE YA SEKONDARI NURU**

**KUMB. Na NSS/J/VOL.12/2026**

**Namba za simu:**

**Mkuu wa Shule: 0765165398/0621954614**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0756321845/0685505130**

**Matron wa Shule: 0768208589**

SHULE YA SEKONDARI NURU

S.L.P. 154 SANYA JUU

TAREHE..............................

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

.................................................................................................................

S.L.P..............................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NURU HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA MKOA WA KILIMANJARO MWAKA ...............**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO Mwaka ............... katika Shule ya Sekondari Nuru Tahasusi ya **PCB** na **PCM** Shule ya Sekondari Nuru ipo katika Wilaya ya SIHA Mkoa Kilimanjaro.

Shule ilipo ukitokea Moshi Mjini unapanda Magari yanayoelekea Sanya Juu, unashuka mwisho wa kituo cha Mabasi Sanya Juu. Kutoka Sanya Juu unaweza kutumia usafiri wa Pikipiki kuelekea eneo la Naibili – Makiwaru kwa gharama isiyozidi Tsh. **5000/=Tu**. Pia upo usafiri wa Mabasi aina ya Costa kutoka Moshi Mjini hadi Naibili nyakati za jioni au Siku za Jumaatano na Jumaamosi.

Mhula wa Masomo unaanza Tarehe ...................Hivyo Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni siku hiyo, Mwisho wa kuripoti ni Tarehe ................

## 1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 1.1 Sare ya Shule

a) Sketi mbili (2) rangi ya kitambaa ni 'kijani cha choroko isiyopauka', aina ya mshono ni rinda box mbele na nyuma(aina ya kitambaa inapatikana Shuleni). **Endapo utakosea rangi, mzazi utawajibika kubadilisha sketi hizo siku ya kuripoti.**

b) Blauzi (mashati) mawili (2) myeupe ya mikono mirefu ya vifungo vya kawaida.

c) Sweta rangi ya 'kijani cha choroko isiyopauka' (inayofanana na rangi ya sketi).

d) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visivyokuwa na visigino virefu na **VISIWE MABUTI.**

e) Soksi jozi mbili (2) nyeupe

f) Blanketi moja (Rangi ya Kijivu)

g) Chandarua, Shuka mbili Rangi **BLUE**

h) Godoro – Ukubwa wa futi "2 1/2" x" 6"

i) Kontena, Kijiko, Kikombe.

j) Sanduku imara la chuma.

k) Koti jeupe kwa ajili ya maandalizi ya masomo ya vitendo(practicals) **lazima**.

l) Kwa wanafunzi wa Tahasusi ya **PCB** waje na 'dissection kit' ambayo itatumika katika masomo ya vitendo (Practicals). **Lazima.**

m) Scientific Calculator (1), unaweza kuipata ukifika Shuleni.

### 1.2 VIFAA VINGINE/ MAVAZI BAADA YA MASOMO

(a) Gauni ya draft ya dark blue mshono wa solo iwe na laining.

(b) Viatu vya michezo, Track suit moja rangi nyeusi yenye Mishirizi ya rangi nyeupe pembeni na tisheti mbili rangi ya blue zisizo na maandishi.

(c) Karatasi A4 ream Mbili (2) kwa Mwaka aina ya **Paperline**

(d) Ndoo mbili moja ya lita 20 na nyingine ndogo ya lita 10, hard broom moja (1), skwiza moja, kishungi, sabuni lita 5 (**dex**),fagio mmoja wa chelewa.

(e) Sabuni, Taulo, Kandambili, Rangi ya Viatu (nyeusi), Mswaki na dawa ya meno, Kanga doti moja.

(f) Toilet papers na Peds za kutosha.

**T-shirt za shule zinapatikana sheleni tsh 15,000/-**

"**VIFAA AMBAVYO HAVIKUTAJWA HAVIRUHUSIWI SHULENI**".

## 2.0 MICHANGO MBALIMABALI:

| **Na** | **AINA YA MICHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| 1 | MICHANGO YA UENDESHAJI WA SHULE | 65,000/= |
| 2 | TAHADHARI | 5,000/= |
| 3. | NEMBO | 5,000/= |
| 4. | KITAMBULISHO CHA SHULE | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Malipo yafanyike kwenye akaunti ya Shule NA. **40101200062 NMB NURU SECONDARY SCHOOL,** Bank Pay in Slip iletwe Shuleni siku ya kuripoti ili ikatiwe risiti.

Siku ya kuripoti aje na muhitasari wa matokeo (result slip) pamoja na cheti cha kuzaliwa.

### 3.0 VITABU VYA MASOMO KWA TAHASUSI(COMBINATIONS)

Mzazi/Mlezi anashauliwa kumnunulia mtoto wake vitabu vya masomo mbalimbali vinavyotumika kulingana na tahasusi aliyopangiwa .

| | |
|---|---|
| Physics | ABC of physics,Fundamentals of physics, ,Understanding mechanics,Engineering physics volume I,Principles of physics class xi and xii (S.Chand). Physics for advanced level secondary school student's book 5 & 6 TIE. |
| Mathematics | Advanced level Maths(C.J.Tranter),Understanding mathematics,Mathematics xi (Chand Mathematics Volume 1 &2,Pure mathematics 1&2(Backhouse),Pure 1 and 2 (Bostock),The core mathematics,Engineering Mathematics, Mathematics Text Book F5 By Tie, Contextial Mathematics Book By P.L Mayombya (New Curiculum). |
| Biology | Biological science(BS),Biological approach,Advanced Biology(Nelson),Advanced Biology volume 1 &2 (S.Chand),Complete Advanced Biology By (Respicius Rwehumbiza). |
| Chemistry | Advanced level General and Physical Chemistry,Conceptual Chemistry volume 1&2,ABC Chemistry(S.Chand).Organic Chemistry. |
| Basic Applied Mathematics | Basic Applied Mathematics TIE |
| A.C | Academic Communication (TIE) |
| HTM | Historia Ya Tanzania Na Maadili, Kidato Cha Tano(TIE) |

**NB.** Mwanafunzi atatakiwa aje na fedha ya matibatu ya kumtosha au kadi ya Bima ya Afya au uje na **Tsh 54,000/-** kwa ajiri ya Bima Ya Afya.

**KARIBU SANA NURU SEKONDARI**

**.................................................**

**MKUU WA SHULE**

## 4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi.

(a) Kuheshimu walimu, Wazazi, Wafanyakazi wasio walimu, Wanafunzi wenzie na jamii yote kwa ujumla.

(b) Kuheshimu na kuthamini kazi aina zote (Ndani na nje ya darasa)

(c) Kushirikiana na kusaidiana katika kazi na masomo.

(d) Kuheshimu na kufuata ratiba ya Shule.

(e) Kila mwnafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na nje ya darasa.

(f) Wito wa mikutano yote. Mfano – Rool call, Ukaguzi (Inspection) na Mstarini (Assemly).

(g) Kutunza muda na ratiba nzima ya Shule

(h) Kufahamu mipaka ya Shule ya kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya Shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

(i) Kuvaa sare ya Shule wakati wote

(j) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari

(k) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo Shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

## 5.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

(a) Wizi, Uasherati Makosa ya jinai na kukataa adhabu.

(b) Kupigana au kunyanyasa wanafunzi wenzie kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.

(c) Ulevi wa aina yoyote mfano Pombe, Sigara, Bangi n.k

(d) Kuharibu kwa makusudi mali za Umma.

(e) Kuoa au kuolewa. Kumpa mimba Msichana/Msichana kupata mimba.

(f) Kudharau Bendera. Wimbo wa Taifa, Wimbo maalum na wimbo wa Shule

(g) Kutohudhuria Masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(h) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

(i) Kumiliki au kupatikana na simu ya mkononi hapa Shuleni.

(j) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi zisizoruhusunjiti ya kiberiti kujificha wakati wote wawapo Shuleni.Huruhusiwi kusuka.

(k) Kufuga ndevu.

(l) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(m) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

## 6.0 USAFI

(a) Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na awe na sare ya Shule illiyo safi wakati wote.

(b) Mwanafunzi atawajibika kwenye usafi wa darasa na maeneo mengine ya Shule.

(c) Mwanafunzi atakayepoteza au kuharibu mali ya Shule atawajibika kulipa.

## 7.0 HAKI YA KUABUDU

Mwanafunzi atambue umuhimu wa uhuru wa kuabudu na kila mwanafunzi ana haki ya kuabudu kwenye Dini yake. Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu Dini ya mwenzake.

## 8.0 ELIMU YA KUJITEGEMEA

Kila mwanafunzi anawajibika kushiriki kwa bidii zote katika shughuli za Elimu ya kujitegemea.

# TAARIFA BINAFSI

1. Jina kamili..........................................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa..............................................................................
3. Mkoa ...................................Wilaya...........................Kabila.......................
4. Taarifa ya kubaini watoto yatima (weka alama ya vema) Baba na mama wote walishafariki ( )

   Baba yupo, mama alishafariki ( )

   Mama yupo, Baba alikwishafariki ( )
5. Jina la Baba/Mlezi Kazi ya baba/Mlezi.......................................................

   Anuani ya anakofanyia kazi S.L.P ..................... Simu ...............................
6. Jina la Mama...............................................Kazi yake................................
   Anuani yake S. L. P .........................................Simu ................................
7. Je wazazi wako huishi pamoja ( )
8. Je wazazi wako wametengana ( )
9. Je wakati wa likizo huwa unaishi na nani?.......................................Unauhusiano gani naye.................................. Anuani yake.......................................................................

   Simu...................................... Wilaya ..........................Mkoa ......................
10. Dini unayoiabudu ..............................Dhehebu ...........................
11. Taarifa za maendeleo zitumwe kwa nani
    Jina.................................................................

    Anuani yake......................................... Simu ........................
12. Wazazi/Ndugu watakao ruhusiwa kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi shuleni ni

    (a) Jina............................................Namba ya simu...........................

    (b) Jina............................................Namba ya simu...........................

    (c) Jina .........................................Namba ya simu............................

    **NB:** Picha zao ziletwe shuleni siku ya kuripoti
13. Ni nani anayekulipia michango ya Shule?
    Jina,..........................................................Anuan........................................
    Anapoishi..................................................Simu.........................................

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITY**

**SIHA DISTRICT COUNCIL**

**REQUST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a Medical Officer in respect of all Form Ones and Five Students who join Secondary School.

**PART A:**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

.................................................................................................................

**STUDENTS FULL NAME**.....................................................................................

Please examine the above named person as to be admitted to Secondary School Education

Signature...................................Designation................................

Name of Head of school Official Stamp.................................................................

**PART B: BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER**

Blood Count (White and red) ...............................................................................

Stool Examination .................................TB Test...............................................

Eye Test......................................Ears .............................................................

Chest. . . . . . . . . . ...................................Spleen......................................................

Abdomen...........................................................................................................

Pregnancy (Girls only) ....................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATIO**N (e g Physical defect or impairment)

.................................................................................................................................

..................................................................................................................

Infection, Chromic disease or Family disease etc

.............................................................................................................................

Please certify that the above is fit to be admitted to secondary school education.

**PART C: MEDICAL OFFICER CERTIFICATION**

I have examined the above person and consider that he/ she is /is not fit physically fit to join secondary education

Medical Officer's Name ......................................... Signature..........................

Official Stamp:

KUTOKA MOSHI MJINI KUELEKEA SHULENI NURU SEKONDARI




HIJABU INAYOKUBARIKA SHULENI




SARE YA SHULE

